HALIUZWI

# Jarida la NEMC

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

ISBN 0856 - 6933 | TOLEO NA. 019 | JULAI - SEPTEMBA, 2025

# BODI MPYA YA NEMC YAHIMIZA UWAJIBIKAJI KWA WATUMISHI NA USAFI WA MAZINGIRA



**Ndani:**

- NEMC YAWAFIKIA WADAU TAKRIBANI 1,450 ELIMU YA MAZINGIRA MAONESHO YA NANENANE
- NEMC YAINGIA MTAANI KIDIGITALI
- NEMC YAJA NA **USAFI KAMPENI 2025**

# YALIYOMO


1. BODI MPYA YA NEMC YAHIMIZA UWAJIBIKAJI KWA WATUMISHI NA USAFI WA MAZINGIRA ..................03
2. NEMC YAKOMESHA UENDESHAJI HOLELA WA KIWANDA BUBU MTAA WA REGENT ESTATE ..................04
3. NEMC YAWATAKA WAMILIKI WA MABASI KUZINGATIA USAFI WA MAZINGIRA BARABARANI ..................05
4. NEMC YAZITAKA WIZARA NA TAASISI ZA UMMA KUTEKELEZA KWA UFANISI SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ..................06
5. NEMC YAFANIKISHA MAFUNZO YA KUJENGEA UWEZO KITAIFA WIZARA, TAASISI NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA JUU YA NYENZO ZA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ..................07
6. NEMC YAPIGA KAMBI SABASABA – YAWAKARIBISHA WANANCHI KUPATA ELIMU YA MAZINGIRA ..................07
7. NEMC YATOA MAFUNZO YA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA KWA WANAFUNZI WA DARTU ..................08
8. NEMC YAUNGANA NA TAASISI NYINGINE KUADHIMISHA SIKU MAALUMU YA MAZINGIRA MAONESHO YA SABASABA 2025 ..................09
9. NEMC YATUNUKU TUZO KWA TANTRADE UTUNZAJI WA MAZINGIRA MSIMU WA SABASABA ..................10
10. NEMC NA WIOMSA WAENDESHA WARSHA KUHUSU UMUHIMU WA VYAKULA VYA BULUU KATIKA LISHE NA USALAMA WA CHAKULA ..................11
11. NEMC YASAJILI MIRADI 8,409 KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE (2021-2025) ..................12
12. DKT. SERERA AVUTIWA NA USHIRIKI WA NEMC MAONESHO YA BIASHARA YA KIMATAIFA BARANI AFRIKA (IATF) ..................13
13. RUVUMA YAFIKIWA ELIMU YA MAZINGIRA - MADINI YA URANIUM ..................14
14. NEMC YAKAGUA MGODI WA 'URANIUM' MKOANI RUVUMA UNAOTARAJIWA KUANZA 2026 ..................15
15. NEMC YAWATAKA WATANZANIA KULINDA VYANZO VYA MAJI ..................16
16. NEMC YAHITIMISHA MAFUNZO YA MRADI WA ECOWEAR KWA WANAFUNZI WA ECCT ..................17
17. NEMC YAPIGA KAMBI VIWANJA VYA NANENANE DODOMA - MAONESHO YA WAKULIMA ..................18
18. NEMC YAWANOA MAWAKILI WA SERIKALI SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ..................18
19. NEMC YAPIGA MARUFUKU UCHIMBAJI WA MCHANGA MTO MPIJI KUEPUSHA UHARIBIFU WA MAZINGIRA ..................19
20. PROFESA MSOFE ARIDHISHWA NA UTENDAJI KAZI NEMC ..................20
21. NEMC YAINGIA MTAANI KIDIGITALI ..................21
22. NEMC, KINONDONI WAADHIMISHA SIKU YA MIKOKO DUNIANI KWA KUPANDA MICHE 1000 ..................22
23. NEMC NA MAZINGIRA PLUS WAFANIKISHA PROGRAMU YA TAKA SIFURI KWA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA YA DAR ES SALAAM ..................23
24. NEMC YAJA NA USAFI KAMPENI 2025 ..................24
25. NEMC YASHIRIKI HAFLA YA UFUNGAJI WA MAONESHO YA NANENANE, DODOMA ..................25
26. NEMC YASHIRIKI HAFLA YA UFUNGAJI WA MAONESHO YA NANENANE, DODOMA ..................26
27. KAULI YA MAZINGIRA YETU ..................27


## UTANGULIZI

### BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilianzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira Na. 19 ya mwaka 1983 kama chombo cha kuishauri serikali juu ya masuala ya utunzaji endelevu wa Mazingira. Baraza lilianza kazi rasmi mwaka 1986. Sheria hiyo Na. 19 ya mwaka 1983 ilifutwa mwaka 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 (Sura 191) ambayo ilianzisha Baraza kwa mara nyingine.

Tangu kuanzishwa kwake, Baraza limekuwa likisimamia na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu suala zima la hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu nchini. Kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria hiyo, madhumuni na sababu za kuanzisha Baraza hili ni kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mazingira katika nyanja kuu nne ikiwa ni pamoja na:-

1. Kutekeleza shughuli za uzingatiaji na utekelezaji (enforcement and compliance) wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;
2. Kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) (Kuratibu, kufanya mapitio ya ripoti za TAM kutoka kwa wenye miradi na kufuatilia utekelezaji wake);
3. Kufanya tafiti za mazingira; na
4. Kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya uamuzi unaohusu mazingira na kusimamia kwa ujumla na kuratibu masuala yote yanayohusu mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Sheria nyingine zozote zilizoandikwa.


**BODI YA UHARIRI:**

**Mwenyekiti:**
Dkt. Menan Jangu

**Mhariri Mkuu:**
Martha P. Kawishe

**Wachangiaji:**
Boniphace Kyaruzi
Tajiri Kihembe
Aziza Muhali
Catherine Ngawi
Alpha Ndahoze

**Msanifu Michoro:**
Blasius Haule

# BODI MPYA YA NEMC YAHIMIZA UWAJIBIKAJI NA USAFI WA MAZINGIRA KWA WATUMISHI



*Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza, Mhandisi Mwanasha Tumbo (aliyesimama) akiongea na Menejimenti na Wajumbe wa Bodi mara baada ya utambulisho. Mbele yake kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi pamoja na Wajumbe wa Bodi.*

Bodi mpya ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ilikutana kwa mara ya kwanza na watumishi wa Taasisi hiyo, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kuimarisha uwajibikaji, mshikamano na ufanisi katika kutimiza malengo yake ya msingi ya kuhifadhi na kusimamia mazingira nchini.

Mkutano huo ulifanyika kwenye kikao cha kawaida cha kila mwezi cha watumishi, ambapo Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Mhandisi Mwanasha Tumbo, aliambatana na wajumbe wengine sita wa bodi na kuwasihi watumishi kuwa mstari wa mbele katika kuonesha mfano wa uadilifu, usafi wa mazingira, na utendaji wenye matokeo.

Akizungumza kwa mara ya kwanza na watumishi hao tangu uteuzi wa bodi hiyo, Mhandisi Mwanasha alisema:

“Ili tuweze kutimiza majukumu yetu ipasavyo kama Taasisi ya mazingira, lazima tuanze na sisi wenyewe kwa kuwa wasafi, wawazi, wenye upendo na tuwe tayari kusikiliza na kushughulikia changamoto za ndani kabla ya kwenda kwa wananchi.”

Alisisitiza kuwa utunzaji wa mazingira unaanzia majumbani kwa Watoto wadogo na kisha kusambaa kwa jamii nzima. Alisema kuwa bodi itasimamia uwazi katika maamuzi, kushirikiana kwa karibu na menejimenti pamoja na kujenga mazingira bora ya kazi kwa watumishi wote.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi, alipopata fursa ya kuzungumza aliikaribisha rasmi Bodi hiyo mpya na kueleza kuwa Menejimenti na watumishi wa NEMC wako tayari kushirikiana kwa dhati ili kuhakikisha taasisi inatekeleza wajibu wake kwa ufanisi.

Bodi hiyo mpya ya Wakurugenzi ya NEMC inatarajiwa kuleta mwelekeo mpya wa kimkakati katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi, hasa katika kipindi hiki ambacho Taifa linakabiliwa na changamoto mbalimbali za kimazingira zikiwemo mabadiliko ya tabianchi, uchafuzi wa mazingira na usimamizi wa taka.



*Bodi ya NEMC na watumishi wakiwa katika kikao kilichofanyika Ukumbi wa Baraza jijini Dar es Salaam mara baada ya Bodi hiyo kutembelea Ofisi za Baraza.*

# NEMC YAKOMESHA UENDESHAJI HOLELA WA KIWANDA BUBU MTAA WA REGENT ESTATE

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilikichukulia hatua za kisheria kiwanda bubu cha SUMING kilichopo Mtaa wa Regent Estate katika Kata ya Mikocheni wilayani Kinondoni kinachofanya shughuli za urejelezaji wa taka hatarishi aina ya simu za kiganjani chakavu katika eneo la makazi ya watu bila kibali cha kukusanya, kurejeleza, kuhifadhi na kusafirisha taka hizo jambo ambalo ni kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.




*Maafisa wa NEMC wakitoa maelekezo kwa mmoja wa wamiliki wa Kiwanda bubu cha SUMING kilichopo Mtaa wa Regent Estate wakati wa ukaguzi wa kiwanda hicho.*

Zoezi hilo lilifanyika mara baada ya timu ya wataalamu wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, TRA pamoja na maafisa wa Serikali ya Mtaa wa Regent kukagua kiwanda hicho na kubaini mapungufu yanayokiuka Sheria ya Usimamizi wa Mazingira nchini.

Akizungumza mara baada ya ukaguzi huo Meneja wa NEMC Kanda ya Mashariki Kaskazini Bi. Glory Kombe alisema ni kosa kisheria kuanzisha kiwanda bila kusajili na kufuata taratibu za kimazingira ikiwepo kuzingatia ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na kupata vibali vya kukusanya na kurejeleza taka za kielectroniki.

Aliutaka Uongozi wa Kiwanda hicho kufika mara moja Ofisi za NEMC ili waweze kupata taratibu zinazotakiwa kufuata wakati wa kuanzisha Mradi ili kuepuka madhara ya kimazingira na Afya ya viumbe hai.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Saad Mtambule aliishukuru NEMC kwa kubaini na kukichukulia hatua Kiwanda hicho na alizitaka Taasisi zote zilizoshiriki ukaguzi wa Kiwanda hicho kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria na miongozo ya Taasisi husika.

Aliongeza kuwa Serikali imeweka Mazingira rafiki yanayovutia uwekezaji nchini hivyo wawekezaji watumie Mazingira hayo vizuri kwa kufuata utaratibu na Sheria ili kuhakikisha shughuli hizo zinafanyika kwa usalama, kuepusha uharibifu wa Mazingira na upotevu wa mapato ya Serikali.

Baraza linaendelea kutoa onyo kali kwa wawekezaji wote wanaoanzisha Viwanda bila kufuata taratibu (Viwanda bubu) ili kuepusha uharibifu wa Mazingira na kulinda Afya ya mazingira na viumbe hai.



*Baadhi ya wafanyakazi wa Kiwanda bubu cha Suming wakiendelea na kazi katika Mazingira ambayo si rafiki na salama katika utendaji wa kazi za Viwanda*



*Timu ya ukaguzi iliyohusisha wataalamu wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, TRA pamoja na maafisa wa Serikali ya Mtaa wa Regent wakijadiliana mara baada ya ukaguzi wa Kiwanda bubu cha Suming*

# NEMC YAWATAKA WAMILIKI WA MABASI KUZINGATIA USAFI WA MAZINGIRA BARABARANI




*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi akizungumza na vyombo vya Habari wakati akitoa wito wa kuwataka wamiliki wa vyombo vya usafiri kuepuka uchafuzi wa mazingira.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) liliwataka wamiliki wa vyombo vya usafiri pamoja na abiria kuzingatia usafi katika mabasi na maeneo ya usafiri barabarani, kwa kuzuia tabia ya kutupa taka nje ya magari na kukojoa mabarabarani.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi alipokuwa akiongea na vyombo vya habari kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kusimamia Mazingira nchini.

Alisema kumekuwepo na mitazamo iliyojengeka kwa abiria wa mabasi makubwa yanayoenda safari ndefu na fupi ya kutokuthamini mazingira na kuwa na tabia ya kutupa taka ovyo na kukojoa barabarani hali inayochafua mazingira, kuharibu hali ya hewa na kuhatarisha afya za jamii.

> **“Ninawahimiza watanzania wote kuwa mabalozi wa usafi katika maeneo wanayopitia. Tukichukua hatua sasa, tunaweza kulinda afya zetu na mazingira kwa vizazi vya sasa na baadae”.**
>
> alisema Dkt. Semesi

“Mazingira safi ni haki ya kila Mtanzania, na ni jukumu letu sote kuhakikisha tunayahifadhi. Kutupa taka nje ya gari na kukojoa barabarani si tu ni tabia mbaya, bali pia ni ukiukwaji wa Sheria za mazingira. Tunawaomba wasafiri na wamiliki wa mabasi kushirikiana nasi kwa kuweka na kutumia vyombo vya kutupa taka ili tukome uchafuzi huu,” alisema Dkt. Immaculate Semesi.

Aidha, NEMC ilitahadharisha kuwa watakaobainika kutupa taka au kukojoa mabarabarani watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwemo faini na adhabu nyingine zinazotolewa kwa mujibu wa Sheria za mazingira.

NEMC imeendelea kutoa simu ya bure 0800 110 115 kwa ajili ya kuripoti uchafuzi wa Mazingira unaosababishwa na abiria, shughuli za binadamu, viwanda bubu au raia ili kuimarisha usimamizi na kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

# NEMC YAZITAKA WIZARA NA TAASISI ZA UMMA KUTEKELEZA KWA UFANISI SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA




*Meneja wa Maeneo Maalumu na Mabadiliko ya Tabianchi (NEMC), Dkt. Careen Anatory Kahangwa akizungumza wakati wa Semina ya kujenga uwezo wa kitaifa juu ya nyenzo za Usimamizi wa Mazingira nchini kwa Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa chini ya Mradi wa EMA.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilizitaka taasisi za umma zikiwemo Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake yanatekelezwa ipasavyo katika maeneo yao ya kazi.

Wito huo ulitolewa mnamo 20 Agosti 2025, katika semina ya mafunzo ya nyenzo za usimamizi wa mazingira chini ya Mradi wa EMA kwa Taasisi za Umma iliyofanyika katika Hoteli ya Midland, Jijini Dodoma kuanzia tarehe 20 hadi 21 Agosti 2025.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi, mgeni rasmi ambaye ni Meneja wa Maeneo Maalumu na Mabadiliko ya Tabianchi, Dkt. Careen Anatory Kahangwa, alisema lengo la semina hiyo ni kuimarisha mbinu za kazi na uwezo wa utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, sambamba na kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi kwa ajili ya usimamizi bora wa mazingira nchini.

"Ushiriki wenu katika kikao hiki ni wa muhimu kwa kuwa unalenga kuhakikisha utekelezaji wa sheria za kitaifa na mikataba ya kimataifa ya mazingira. Hii itawezekana tu iwapo mtayapokea mafunzo haya kwa umakini na kuyazingatia ili kujengewa uwezo wa kutosha katika kusimamia vyema mazingira," alisema Dkt. Kahangwa.

Kwa upande wake, Afisa Mazingira Mkuu wa NEMC na Mratibu Mkuu wa Mradi wa EMA, Bw. Paul Mashaija Kalokola alieleza kuwa kumekuwa na uhitaji mkubwa wa kujengea uwezo taasisi mbalimbali ili wadau waweze kufahamu na kutumia nyenzo muhimu za usimamizi wa mazingira nchini.

Aliongeza kuwa changamoto kubwa ni udhaifu wa baadhi ya taasisi katika kutekeleza ipasavyo Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, hali iliyosababisha kuanzishwa kwa mradi huo wa miaka mitatu unaosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, wenye lengo la kuimarisha uwezo wa wadau wote nchini katika kusimamia mazingira kwa ufanisi.



*Washiriki wa Semina ya kujenga uwezo wa kitaifa juu ya nyenzo za Usimamizi wa Mazingira nchini chini ya Mradi wa EMA kwa Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa wakiwa katika picha ya Pamoja mara baada ya awamu ya kwanza ya Semina kuisha.*

# NEMC YAFANIKISHA MAFUNZO YA KUJENGEA UWEZO KITAIFA WIZARA, TAASISI NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA JUU YA NYENZO ZA USIMAMIZI WA MAZINGIRA




*Afisa Mazingira Mkuu wa NEMC ambaye pia ni Mratibu Mkuu wa Mradi wa EMA, ndugu Paul Kalokola (anayeongea) akizungumza katika semina ya kujenga uwezo wa kitaifa juu ya nyenzo za usimamizi wa Mazingira nchini.*

Baraza za la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC lilifanikisha mafunzo ya kujenga uwezo wa kitaifa juu ya nyenzo za Usimamizi wa Mazingira nchini kwa Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za mitaa.

Mafunzo hayo ya siku mbili yalianza 20-21 Agosti, 2025 katika Hoteli ya Midland Jijini Dodoma huku yakihusisha uwasilishaji wa mada na majadiliano, pamoja na maswali na majibu ya papo kwa papo.

Aidha mafunzo hayo yalilenga kuhakikisha Taasisi zote za umma na Mamlaka za Serikali za mitaa zinahakikisha matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake yanatekelezwa ipasavyo

Baadhi ya mada zilizowasilishwa ni pamoja na hali ya udhibiti wa taka za kielekroniki katika miji na manispaa, changamoto na fursa zilizopo katika taka za kielektroniki, Udhibiti wa madampo haramu, Mpango mkakati wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira, Mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii pamoja na Kaguzi za Mazingira pamoja na mchakato wa kupata vibali vya taka hatarishi pamoja na changamoto zilizopo katika udhibiti wake.

Katika kuhitimisha mafunzo hayo baadhi ya washiriki walilishukuru Baraza kwa mafunzo hayo huku wakieleza kuwa wamepata mbinu mpya ambazo awali hawakuwa nazo katika swala zima la Usimamizi wa Mazingira nchini.

# NEMC YAPIGA KAMBI SABASABA – YAWAKARIBISHA WANANCHI KUPATA ELIMU YA MAZINGIRA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilipiga kambi viwanja vya sabasaba maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ili kutoa elimu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira kwa wananchi waliotembelea banda hilo katika Jengo la Karume.

Akizungumza katika maonesho hayo, Mhandisi Mwandamizi wa NEMC, Bw. Haji Kiselu, alisema Baraza limejipanga kikamilifu kuhakikisha elimu ya mazingira iliyo jumuishi inamfikia kila mwananchi, ili kwa pamoja tuweze kuyasimamia kwa maendeleo endelevu nchini.

Kwa upande wake, Mhandisi wa NEMC, Bw. Peres Ntinginya, alipozungumza, alisisitiza kuwa utunzaji wa mazingira ni jukumu la kila mmoja hivyo yapasa kuwajibika na kutoa wito kwa wananchi kutumia nishati safi ya kupikia kwa kuwa matumizi yake husaidia kulinda afya ya binadamu na viumbe hai, kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa, pamoja na kuhifadhi mazingira kwa ujumla.

Naye Mkazi wa Rufiji, Bw. Ayubu Njanja, alisema elimu aliyoipata kutoka kwa Maafisa wa Baraza imempa mwongozo sahihi wa kuzingatia katika kuhakikisha mazingira yanasimamiwa hasa katika shughuli za kilimo.




*Bw. Ayubu Njanja akipatiwa elimu ya mazingira kutoka kwa wataalam wakati wa msimu wa maonesho ya 49 ya Sabasaba.*

# NEMC YATOA MAFUNZO YA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA KWA WANAFUNZI WA DARTU



*Afisa Mazingira Mwandamizi Bw. Emmanuel Salyeem akiwasilisha mada ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Tumaini Dar es Salaam (DARTU) katika Ukumbi wa Mikutano NEMC jijini Dar es salaam.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) liliendesha mafunzo maalum ya kuwajengea uelewa kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) wanafunzi wa mwaka wa tatu wa kada ya ualimu kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini Dar es Salaam (DARTU).

Mafunzo hayo yalifanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa NEMC uliopo jijini Dar es Salaam, na yaliongozwa na Afisa Mazingira Mwandamizi, Bw. Emmanuel Salyeem.

Katika mafunzo hayo, Bw. Salyeem alitoa wasilisho lililojikita katika kuelezea mchakato mzima wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira, akitoa mifano hai ya namna Baraza linavyoendesha mchakato mzima wa Tathmini hiyo kwenye miradi mikubwa, ya kati na midogo. Alisisitiza umuhimu wa TAM katika kulinda afya ya viumbe hai wote pamoja na mazingira kwa ujumla.

Kupitia mafunzo haya, wanafunzi walipata nafasi ya kuelewa kwa kina majukumu ya NEMC na mchango wa Tathmini ya kimazingira katika maendeleo endelevu ya Taifa.

NEMC inaendelea kutoa wito kwa Taasisi za elimu, vikundi vya kijamii na wadau mbalimbali kufika katika ofisi za Baraza kwa ajili ya kupata elimu ya uhifadhi wa mazingira na kujifunza namna bora ya kushiriki katika kulinda mazingira yetu.



*Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Tumaini Dar es Salaam (DARTU) wakiwa katika picha ya pamoja na Afisa Mazingira Mwandamizi Bw. Emmanuel Salyeem mara baada ya kupata mafunzo.*

# NEMC YAUNGANA NA TAASISI NYINGINE KUADHIMISHA SIKU MAALUMU YA MAZINGIRA MAONESHO YA SABASABA 2025




*Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhandisi Cyprian Luhemeja akimkabidhi zawadi na cheti cha heshima Mshindi wa kwanza wa mashindano ya 'Mazingira Challenge' Bw. Paulo Dotto Masele yaliyofanyika katika msimu wa sabasaba.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC Julai 6, 2025 liliungana na Taasisi mbalimbali kuadhimisha Siku maalumu ya Mazingira iliyotengwa kwa mara ya kwanza kwenye Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (sabasaba) 2025.

Mgeni rasmi katika Maadhimisho hayo alikuwa ni Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhandisi Cyprian Luhemeja huku tukio hilo likibebwa na Kauli mbiu isemayo "Matumizi ya Nishati safi na utunzaji wa Mazingira kwa ustawi wa Tanzania bora".

Akizungumza katika hotuba yake Mhe. Cyprian Luhemeja aliitaka siku hiyo itengwe rasmi kuwa siku maalumu ya Mazingira kila mwaka katika maonesho hayo kuanzia maonesho ya 50 ya biashara ya kimataifa (sabasaba).

Sambamba na hilo alisisitiza watanzania wote kutunza Mazingira kwa kuwa Mazingira yaliumbwa kwanza kisha mwanadamu akaumbwa baadae ili ayatunze, ayahifadhi na kuyalinda.

"Hii duniani ilianza kwa kutengenezewa Mazingira, mwanadamu ameumbwa wa mwisho baada ya Mazingira kutengenezwa, na mwanadamu alipoumbwa alipewa kazi ya kuyatunza na kuyahifadhi Mazingira lakini mwanadamu anayaharibu kwa uchafuzi na ukataji wa miti.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi alipozungumza aliwapongeza washindi wa Mazingira Challenge iliyofanyika kwa lengo la kuibua ari ya watanzania kuona umuhimu wa kuhifadhi na kusimamia mazingira nchini.

Maadhimisho hayo yaliyoambatana na ugawaji wa zawadi kwa washindi wa mazingira challenge iliyohusu upigaji picha wa eneo zuri la mazingira yalipambwa na mabalozi wa Mazingira pamoja na watumbuizaji nguli akiwemo Mrisho Mpoto pamoja na Mr. Tree na kuhudhuriwa na Viongozi mbalimbali akiwemo Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Menejimenti ya NEMC, TANTRADE, STAMICO, Wanawake na Samia, Shirika la PUMA pamoja na wananchi waliotembelea maonesho ya sabasaba.

# NEMC YATUNUKU TUZO KWA TANTRADE UTUNZAJI WA MAZINGIRA MSIMU WA SABASABA




*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi akimkabidhi tuzo Mkurugenzi Mkuu wa TANTRADE Bi. Latifa Khamis kwa kusimamia utunzaji wa Mazingira msimu wote wa maonesho katika hafla ya kufunga maonesho ya sabasaba 2025*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilitunuku tuzo ya heshima kwa Mamlaka ya maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) kuhusu utunzaji wa Mazingira, katika hafla ya kufunga maonesho ya biashara kimataifa ya 49 iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.

Akikabidhi tuzo hiyo, kwa Mkurugenzi Mkuu wa TANTRADE Bi. Latifa Khamis, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi alisema NEMC alikabidhi tuzo hiyo kwa kutambua tano bora za utunzaji na usafi wa Mazingira uliosimamiwa nao katika kipindi chote cha Maonesho ya sabasaba 2025.

Dkt. Semesi aliziainisha tano bora hizo ambazo ni; Ubunifu siku maalumu ya Mazingira iliyoadhimishwa tarehe 06.07.2025, mandhari ya maonesho kuwa safi na ya kupendeza kipindi chote cha maonesho, kuhamasisha matumizi ya Nishati safi, kuhamasisha washiriki kutumia bidhaa ambazo ni rafiki kwa Mazingira na kufaulu kudhibiti taka licha ya idadi kubwa ya watu kutembelea maonesho hayo.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Viongozi mbalimbali Pamoja na Wakuu wa Serikali akiwemo Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa ambaye ndiye alikuwa mgeni rasmi na aliyefunga maonesho ya sabasaba 2025, Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Seleman Jafo pamoja na viongozi wengine.

Maonesho ya biashara ya kimataifa kwa mwaka 2025 yalibeba Kaulimbiu mbiu isemayo "***Maonesho ya biashara ya Kimataifa Sabasaba, Fahari ya Tanzania***".

Aidha, yalihudhuriwa na takribani nchi 22 na asilimia 70 ya wawekezaji waliweza kufikia malengo yao na kuongeza idadi ya wadau na masoko.

Baraza linaendelea kuhimiza wawekezaji na watanzania wote kwaujumla kuendelea kuzingatia kanuni na miongozo ya utunzaji wa Mazingira kwa ajili ya Tanzania endelevu, safi na salama.



*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi akiwa na baadhi ya washiriki katika hafla ya kufunga maonesho ya sabasaba 2025.*

# NEMC NA WIOMSA WAENDESHA WARSHA KUHUSU UMUHIMU WA VYAKULA VYA BULUU KATIKA LISHE NA USALAMA WA CHAKULA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Taasisi ya WIOMSA (West Indian Ocean Marine Science Association) waliendesha Warsha kwa wadau wa Sekta mbalimbali za Serikali, binafsi na za kijamii kuhusu mchango wa vyakula vya baharini, kwenye mito na maziwa "Blue foods" katika lishe na usalama wa chakula.

Warsha hiyo ya Siku mbili ilifanyika kuanzia tarehe 21 hadi 22 Julai, 2025 katika Ukumbi wa Hoteli ya Tanga Resort Mkoani Tanga.

Akizungumza katika ufunguzi wa Warsha hiyo Mgeni rasmi, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa buluu na Uvuvi Zanzibar Bw. Zahor Kassim Mohamed alieleza kuwa vyakula vya buluu "Blue foods" ni muhimu sana katika lishe bora na usalama wa chakula.

"Vyakula vya buluu "Blue foods" kama vile samaki, dagaa, kaa, majongoo wa baharini, mwani na viumbe wengine vinamchango mkubwa katika lishe bora, usalama wa chakula, uchumi wa Kaya na ajira." Alisema Bw. Zahor Mohamed.



*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi akizungumza wakati wa Warsha ya mchango wa vyakula vya baharini "Blue foods" katika lishe na usalama wa chakula iliyofanyika Mkoani Tanga.*

Akiongea na Waandishi wa habari mara baada ya awamu ya kwanza ya warsha hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi alisema lengo kuu la Warsha hiyo ni kuhamasisha juu ya umuhimu wa vyakula vya baharini, katika mito na maziwa "Blue foods" katika lishe bora kwani vyakula hivyo vina manufaa makubwa katika Afya ya mwanadamu na hivyo kujenga Taifa lenye watu wenye uelewa na kuweza kujitegemea.




*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa buluu na Uvuvi Zanzibar Bw. Zahor Kassim Mohamed (Katikati) katika picha ya pamoja na watumishi wa taasisi zilizoshiriki Warsha ya mchango wa vyakula vya baharini "Blue foods" katika lishe na usalama wa chakula. Wapili kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi na wa pili kushoto ni Mkurugenzi wa Taasisi ya WIOMSA Dkt. Arthur Tude*

Akiwasilisha mada Mkurugenzi wa Taasisi ya WIOMSA Dkt. Arthur Tude alisema Taasisi hiyo imejikita katika tafiti za kuboresha lishe bora na kuelimisha jamii kuhusu vyakula vya baharini, hivyo iliamua kushirikiana na NEMC pamoja na Taasisi nyinginezo kuhamasisha jamii juu ya uvunaji wa vyakula vya baharini vyenye lishe bora.

Aidha, Zahor alisisitiza kuwa ni muhimu Sekta zote binafsi na za Serikali, Taasisi na washirika wa maendeleo na jamii za uvuvi kuhakikisha kuwa "blue food" zinachangia kwa ufanisi kutokomeza njaa, kuongeza kipato na kulinda Mazingira ya bahari, mito na maziwa ambavyo ni rasilimali muhimu za kufuga vyakula buluu.

Aliongeza kuwa, licha ya changamoto zinazokabili ustawi wa vyakula vya buluu, Serikali imeweza kuimarisha Sekta hiyo ikiwa ni pamoja na kuwezesha ufugaji samaki katika mabwawa ya kisasa, kuwezesha vikundi vya Wanawake na vijana katika mnyororo wa thamani wa mazao ya maji, kushiriki katika juhudi za kimataifa na kikanda kama vile Blue Economy na mabadiliko ya mifumo ya chakula duniani.

# NEMC YASAJILI MIRADI 8,409 KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE (2021-2025)

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) katika kipindi cha miaka minne (2021–2025), imepiga hatua kubwa katika usimamizi wa mazingira nchini, ambapo jumla ya **miradi 8,409** imesajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa uchambuzi wa kimazingira.

Kati ya miradi hiyo **6,040** imefanyiwa **Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA)**, ambayo ni hatua muhimu inayotathmini athari za kimazingira kabla ya mradi kuanza kutekelezwa na **2,369** imepitiwa kupitia **kaguzi za mazingira (EA)**, ambazo hufanyika mara baada ya mradi kuanza ili kuhakikisha uzingatiaji wa taratibu za kimazingira.

Kadhalika jumla ya **vyeti 4,912 vya mazingira** vimetolewa kwa miradi iliyokidhi matakwa ya Sheria na taratibu, ambapo **4,164** kati ya hivyo vilitokana na tathmini za Athari kwa Mazingira (EIA) na **748** vilitolewa baada ya kufanyika kwa kaguzi za mazingira.


Katika kuhakikisha utekelezaji wa Sheria na miongozo ya mazingira inazingatiwa,jumla ya wataalamu elekezi **1,513** hadi sasa wamesajiliwa. Hawa ndio washauri wanaochangia kwa kiasi kikubwa katika kufanya tathmini, kutoa ushauri wa kitaalamu, na kusimamia utekelezaji wa miradi kwa kuzingatia uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Kwa upande wa **Utafiti/Tathmini** kwa kipindi cha miaka minne zimefanyika 21, zikiwa na lengo la kutoa ushahidi wa kisayansi na mapendekezo ya kishera ili kuboresha mifumo ya usimamizi wa mazingira nchini.

Mafanikio haya ni ishara ya jitihada za pamoja kati ya serikali, sekta binafsi, wataalamu wa mazingira na wananchi kwa ujumla katika kulinda na kuhifadhi mazingira kwa maendeleo endelevu.

**"Hatua hizi ni sehemu ya dhamira ya nchi kuhakikisha maendeleo hayapingani na uhifadhi wa mazingira. NEMC inaendelea kuhimiza uwekezaji rafiki wa mazingira kupitia mifumo madhubuti ya Tathmini na usimamizi."**

## MIRADI ILIYOSAJILIWA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2021-2025






# DKT. SERERA AVUTIWA NA USHIRIKI WA NEMC KWENYE MAONESHO YA BIASHARA YA KIMATAIFA BARANI AFRIKA (IATF)




*Naibu Katibu Mkuu wa Viwanda na Biashara, Dkt. Suleiman Serera (wapili kulia) akizungumza na Mhandisi Mazingira (NEMC) Peres Ntinginya katika maonesho ya Biashara ya Kimataifa Barani Afrika yanayotambulika kama Intra African Trade Fair (IATF) yaliyofanyika jijini Algiers nchini Algeria kuanzia Septemba 4-10, 2025.*

Naibu Katibu Mkuu wa Viwanda na Biashara, Dkt. Suleiman Serera alilipongeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa namna ambavyo linatoa elimu kwa wadau mbalimbali wakiwemo wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali barani Afrika kwenye Maonesho ya Biashara ya Kimataifa Barani Afrika yanayotambulika kama Intra African Trade Fair (IATF) yaliyofanyika jijini Algiers nchini Algeria kuanzia Septemba 4-10, 2025.

Dkt. Serera ambaye alikuwa Mkuu wa msafara wa Ujumbe wa Tanzania ulioshiriki Maonesho hayo, alitoa pongezi hizo alipofika Banda la Tanzania akiambatana na mwenyeji wake ambaye ni Balozi wa Tanzania nchini Algeria, Mhe. Iman S. Njalikai.

"Uchumi tunaoutaja ni Uchumi wa Viwanda, lakini Viwanda tunavyohitaji ni viwanda vinavyozingatia Uhifadhi wa Mazingira, hivyo basi NEMC kwa kuja hapa wanawaambia wawekezaji waje lakini yapo ya kuzingatia kuhusu Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira" alisema Dkt. Serera.

"NEMC inalo jukumu la kuendelea kutoa elimu na nilichopenda zaidi ni kwamba hakuna urasimu, nimeona hapa taarifa zote unaweza kuzisoma na kuzipata kupitia "QR Code" kabla hata ya kuja kuwekeza Tanzania, Na hapa niwapongeze sana NEMC kwa namna mnavyofanya kazi vizuri na muendelee hivyo kwani Mazingira ni uhai ni lazima tuyatunze ili yatutunze" Amesisitiza Dkt. Serera.

Naye Balozi wa Tanzania nchini Algeria, Mhe. Imani S. Njalikai alizitaka Taasisi zilizoshiriki Maonesho hayo kuitumia fursa hiyo vizuri hasa katika maeneo ambayo Algeria inafanya vizuri kwenye sekta ya nishati ambayo ni pamoja na gesi, mafuta, mbolea na sekta ya madawa (pharmaceutical) ambayo ni pamoja na mafunzo kwenye maeneo hayo.

NEMC ikiwa ni moja ya Taasisi zilizoshiriki Maonesho hayo iliwakilishwa na Mhandisi Mkuu, Peres Ntinginya na Afisa Uhusiano na Mawasiliano, Bw. Tajiri Kihemba. Taasisi nyingine zilizoshiriki ni pamoja na TANTRADE ambazo ziliratibu maonesho hayo kwa upande wa Tanzania ni TMDA, FCC, TISEZA, PURA, TFS, ZIPA.




*Ujumbe wa Tanzania ukiwa katika picha ya pamoja na Naibu Katibu Mkuu wa Viwanda na Biashara, Dkt. Suleiman Serera katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa Barani Afrika yanayotambulika kama Intra African Trade Fair (IATF) yaliyofanyika jijini Algiers nchini Algeria kuanzia Septemba 4-10, 2025.*

# RUVUMA YAFIKIWA ELIMU YA MAZINGIRA - MADINI YA URANIUM



*Meneja Kanda ya Kusini (NEMC) Bw. Boniface Guni akiwasilisha mada kwa wanakijiji wa Mandela-Likuyu Wilayani Namtumbo Mkoani Ruvuma wakati wa utoaji wa elimu ya Mazingira na Afya kufuatia Uchimbaji mkubwa wa madini ya 'Urunium' utakaoanza mwakani 2026*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilitoa elimu ya kimazingira na afya kwa vijiji viwili vya Mtonya na Mandela-Likuyu katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo Mkoani Ruvuma kufuatia Mradi wa Uchimbaji wa Madini aina ya 'Uranium' ulitarajiwa kuanza katika mgodi ulio karibu na vijiji hivyo.

Elimu hiyo ilitolewa kwa wananchi kuanzia 8-9 Septemba, 2025 kwa vijiji hivyo huku ikifuatiwa na ukaguzi uliofanyika katika mgodi huo ambapo ilikuwa hatua ya awali ya kuelimisha jamii na wawekezaji kabla ya Mradi huo kuanza ambapo ni maagizo yaliyotolewa na Serikali ili kuhakikisha jamii inatambua uwepo wa Mradi huo na kuhakikisha jamii haiathiriki na Mradi huo.

Akizungumza katika utoaji wa elimu hiyo kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi, Kaimu Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria (NEMC) Bw. Jamal Baruti aliutaka Uongozi wa vijiji hivyo kutumia Kamati za Mazingira na kushirikiana na Serikali kuendelea kuelimisha jamii juu ya maswala ya Mazingira na Afya ya jamii yanayoweza kusababishwa na Mradi huo.

Kwa upande wake, Meneja Kanda ya Kusini (NEMC) Bw. Boniface Guni aliwataka wakazi wa vijiji hivyo kuchangamkia fursa za ajira katika Mradi huo huku wakizingatia ulinzi wa Afya zao na Mazingira.

Aidha Kaimu Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria NEMC Bw. Jamal Baruti alisema NEMC itaendelea na ufuatiliaji wa maswala ya kimazingira kwa kushirikiana na Taasisi nyingine huku akiitaka Kampuni ya Mantra TZ LTD ya Uchimbaji katika mgodi huo kutambua haki za wakazi wa vijiji hivyo na kuchangia shughuli za maendeleo ya wakazi wa vijiji hivyo kama manufaa ya Mradi huo.



*Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria (NEMC) Bw. Jamal Baruti akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wanakijiji na Viongozi wa Kijiji cha Mtonya Wilayani Namtumbo Mkoani Ruvuma mara baada ya kuwapatia elimu ya Mazingira na Afya kufuatia Uchimbaji mkubwa wa madini ya 'Urunium' utakaoanza mwakani 2026*

# NEMC YAKAGUA MGODI WA 'URANIUM' MKOANI RUVUMA UNAOTARAJIWA KUANZA 2026

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilifika na kukagua Mgodi wa madini aina ya Uranium uliopo katika Wilaya ya Namtumbo Mkoani Ruvuma ambao ulikuwa katika Uchimbaji mdogo wa majaribio huku Uchimbaji mkubwa ukitarajiwa kuanza mwaka 2026.

NEMC ilifika na kufanya Ukaguzi katika Mgodi huo na kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha shughuli za Uchimbaji katika Mgodi huo haziathiri Mazingira, Viumbe hai na wakazi wa jirani na Mgodi huo ikiwa ni agizo la Serikali.

Awali NEMC ilianza kwa kutoa elimu ya Mazingira na Afya kwa wakazi wa vijiji vilivyo karibu na Mgodi huo ili kuwajengea uelewa kuhusiana na madini ya 'Uranium' jinsi yanavyoweza kuhatarisha afya na Mazingira ikiwa hayata chakatwa na kudhibitiwa kwa umakini.

Akizungumza katika Ukaguzi huo Kaimu Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria Bw. Jamal Baruti alisema NEMC ilifika katika Mgodi huo kufanya Ukaguzi ili kutathmini ikiwa wawekezaji katika Mgodi huo wamekidhi na kuzingatia miondombinu ya Mazingira ambayo haita haribu Mazingira, kuhatarisha usalama wa wakazi na wafanyakazi katika Mgodi huo kabla Uchimbaji mkubwa haujaanza.

Aidha Bw. Baruti alieleza kuwa Mradi wa Mgodi huo utakuwa na uwezo wa kuzalisha tani elfu 27 kwa siku na utakuwa ni Mradi mkubwa wa Uchimbaji madini nchini ukilinganisha na Miradi mingine nchini Tanzania.

Aliongeza kuwa Tanzania itakuwa nchi ya nne ya uzalishaji wa madini ya 'Uranium' Duniani huku akiwasisitiza wawekezaji na wananchi kuzingatia uhifadhi Mazingira na si tu kuangalia manufaa ya Mgodi huo.

Kwa upande wake Meneja Kanda ya Kusini (NEMC) Bw. Boniface Guni alisema ziara hiyo iliwasaidia NEMC kupata picha ya Mradi huo ambayo itawasaidia kusimamia Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na jamii ipasavyo.

Naye Mwenyekiti wa Kitongoji cha Buchushu Kijiji cha Iguseka Bw. Omary Rashid aliishukuru NEMC kwa kuwapatia elimu hiyo adhimu ya Mazingira wakazi wa vijiji hivyo ambayo ni muhimu katika utunzaji wa Mazingira na Afya ya binadamu.



*Timu ya wataalamu wa Mazingira kutoka NEMC na Kampuni ya Uchimbaji ya MANTRA wakikagua moja ya mlima wenye madini ya 'Urunium' wakati wa ukaguzi wa Mgodi huo. Wa pili kulia ni Kaimu Meneja wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria (NEMC) Bw. Jamal Baruti.*



*Timu ya wataalamu wa Mazingira kutoka NEMC na Kampuni ya Uchimbaji ya MANTRA wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya ukaguzi wa Mgodi wa madini ya 'Urunium' katika eneo la Mto Mkuju Wilayani Namtumbo Mkoani Ruvuma. Wa katikati ni Kaimu Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria (NEMC) Bw. Jamal Baruti na kushoto kwake ni Meneja wa Mradi, Bw. Beria Vorster*

# NEMC YAWATAKA WATANZANIA KULINDA VYANZO VYA MAJI

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) liliwahimiza watanzania kuchukua hatua madhubuti za kulinda na kuhifadhi mazingira asilia, ili kuzuia uharibifu wa vyanzo vya maji kwa ajili ya ustahimilivu na uendelevu wa rasilimali maji, ambayo ni muhimu kwa maisha ya binaadamu, uchumi wa viwanda na kilimo pamoja na uhai wa viumbe vyote.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mhandisi wa Mazingira na Miundombinu ya Maji, Mhandisi Boniphace Kyaruzi, alisema kuwa mazingira ya vyanzo vya maji nchini yanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uharibifu wa uoto wa asili unaotokana na ukataji miti holela, kilimo ndani ya mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji, uchafuzi wa vyanzo utokanao na matumizi ya mbolea za kisasa, shughuli za viwanda pamoja na utupaji holela wa taka za majumbani.

Alieleza kuwa ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha kuwa mazingira asilia ya vyanzo vya maji yanalindwa kwa lengo la kuhifadhi rasilimali hiyo muhimu kwa maisha ya binadamu na viumbe hai wengine.

Tunaweza kurejesha vyanzo vya maji vilivyopotea kwa kupanda miti na kurejesha uoto wa asili, pamoja na kudhibiti shughuli za kibinadamu katika maeneo ya vyanzo vya maji. Ni muhimu kuepuka kilimo ndani ya mita sitini kutoka kwenye vyanzo hivyo, kudhibiti taka za majumbani kwa kuzitupa katika maeneo rasmi, na kuhakikisha maji taka kutoka viwandani yanatibiwa kabla ya kutiririshwa," alisema Mhandisi Kyaruzi.

Aidha, aliwataka Watanzania kubadili mitazamo na tabia kuhusu usimamizi wa taka na uhifadhi wa mazingira ili kuepusha uchafuzi wa vyanzo vya maji, ambavyo ni msingi wa maisha kwa viumbe hai wote.

"Ni muhimu sana tutunze vyanzo vya maji. Maji ni uhai bila maji hatuwezi kupika, kunywa, kufanya usafi wala kuendesha shughuli za kiuchumi kama vile viwanda. Hata mazingira yenyewe hayawezi kustawi bila maji," amesisitiza.

Mhandisi Kyaruzi amebainisha kuwa Tanzania imebarikiwa kuwa na vyanzo vingi vya maji.




*Mhandisi wa Mazingira na Miundombinu ya Maji (NEMC) Mhandisi Boniphace Kyaruzi akizungumza na vyombo vya habari kuhusu umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji.*

# NEMC YAHITIMISHA MAFUNZO YA MRADI WA ECOWEAR KWA WANAFUNZI WA ECCT



*Meneja Utekelezaji wa Sheria (NEMC) Bi. Amina Kibola (wa pili kulia) kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, akimkabidhi cheti mmoja wa wahitimu wa mafunzo ya Mradi wa ECOWEAR katika hafla ya mahafali hiyo.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC kwa kushirikiana na Taasisi ya ECCT (Environment Conservation Community of Tanzania) walihitimisha takribani wanafunzi 22 wa Mradi wa '***Ecowear***' waliokuwa wakipatiwa mafunzo yaliyobeba agenda ya mazingira kwenye ubunifu na Sanaa ya mitindo yenye lengo la kujenga ujasiriamali wa kijani, kupambana na taka ngumu za Sekta ya nguo na mitindo sambamba na matumizi endelevu ya rasilimali.

Mafunzo ya Mradi huo yalijikita kufundisha juu ya ubunifu wa bidhaa mbalimbali kupitia nguo zilizotumika na mabaki ya vitambaa ambapo ni Utekelezaji wa dhana ya ***Punguza, Tumia tena na Rejeleza*** kwa mustakabali wa utunzaji wa Mazingira na fursa za kiuchumi.

Akizungumza katika mahafali hayo, mgeni rasmi ambaye ni Meneja Utekelezaji wa Sheria (NEMC) Bi. Amina Kibola kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi aliipongeza Taasisi ya ECCT na wahitimu wote kwa kufanikisha mafunzo hayo na kuwataka kuyazingatia kwa manufaa ya kiuchumi na Mazingira.

"Mmepata elimu, ujuzi, maarifa, mmeelewa changamoto za mazingira, sasa ni wakati wa kupeleka hayo yote kwa jamii zetu. Tuna matarajio makubwa kwenu kama mabalozi wa mitindo endelevu na watetezi wa mazingira. endeleeni kushirikiana, kupeana maarifa na kuamini kuwa sauti zenu na kazi zenu zinaweza kuleta mabadiliko." Alisisitiza Bi. Amina.

Bi. Amina pia alitumia fursa hiyo kutoa elimu kuhusu katazo la vifungashio vya plastiki kwa mujibu wa Kanuni ya katazo hilo na kuwataka wahitimu wa mradi huo kubuni na kutengeneza vifungashio vinavyoenda sambamba na mustakabali wa utunzaji wa Mazingira.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa ECCT, Bi. Lucky Michael alilishukuru Baraza kwa mchango wake kufanikisha kuhitimisha wanafunzi hao huku akiainisha mafanikio ya Mradi huo kuwa ni pamoja na kujengeana uwezo kwa wanafunzi hao katika suala zima la ubunifu na mitindo, kukusanya takribani tani 2 za mabaki ya nguo na vitambaa kuzigeuza kuwa bidhaa zenye ubora pamoja na kuhamasisha jamii kupunguza taka na kutumia mitindo endelevu.

# NEMC YAPIGA KAMBI VIWANJA VYA NANENANE DODOMA - MAONESHO YA WAKULIMA




*Timu ya maafisa wa NEMC ikimsikiliza mgeni aliyetembelea banda lake katika maonesho ya wakulima, Nanenane 2025 katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma .*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilipiga kambi katika Viwanja vya Nanenane, Nzuguni jijini Dodoma kuelimisha watanzania umuhimu wa kuzingatia kilimo kinachohifadhi mazingira katika msimu huu wa Nanenane wenye kaulimbiu isemayo "Chagua viongozi Bora kwa maendeleo ya kilimo, mifugo na uvuvi."

Elimu iliyotolewa katika Banda la NEMC ni pamoja na umuhimu wa kuzingatia ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM), katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki, athari za uchafuzi wa vyanzo vya maji, umuhimu wa kuzingatia kilimo hifadhi, umuhimu wa kulipa ada za mazingira, pamoja na elimu ya urejelezaji wa taka.

NEMC iliwakaribisha wakulima, wafugaji na wavuvi pamoja na wadau wengine wa Mazingira katika Banda lake kupata elimu kwa maendeleo endelevu ya mazingira nchini.

# NEMC YAWANOA MAWAKILI WA SERIKALI SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilitoa mafunzo ya uelewa wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na utekelezaji wa majukumu yake kwa mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

Akizungumza katika Mafunzo hayo tarehe 3 Septemba, 2025 Mkurungenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Semesi alisema kuwa wameandaa mafunzo hayo kwa lengo la kujengeana uelewa wa kisheria katika usimamizi wa mazingira nchini pamoja na kuboresha mahusiano mazuri katika Usimamizi na Utekelezaji wa Sheria za Mazingira nchini.

Akifungua Mafunzo hayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari alisema wanasheria hao wanatakiwa kuwa walinzi na kuongeza umakini katika kutoa ushauri wa sheria za mazingira kwa maslahi ya nchi.

“Natambua zipo changamoto wakati wa utekelezaji ,mfano uelewa mdogo wa masuala ya mazingira hivyo tunawajibu wa kuzibadili changamoto hizi na kuzifanya fursa kwa kuimarisha nafasi ya NEMC katika kusimamia sheria katika sekta ya mazingira.”Alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alilishukuru Baraza na kueleza kuwa mafunzo hayo yataongeza uelewa kwa Mawakili wa Serikali hivyo kuwasaidia wakati watakapokuwa wanatoa Ushauri wa Kisheria na Upekuzi wa Mikataba inayohusu hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini.



*Mawakili wa Serikali wakiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi (wa pili kulia walioketi) kushoto kwake ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari mara baada ya mafunzo hayo. Wa kwanza kulia ni Mkurugenzi wa Sheria (NEMC), Bw. Joannes Karungura.*

# NEMC YAPIGA MARUFUKU UCHIMBAJI WA MCHANGA MTO MPIJI KUEPUSHA UHARIBIFU WA MAZINGIRA



*Meneja Uzingatiaji wa Sheria (NEMC) Bw. Hamadi Taimuru akizungumza na kutoa zuio kwa baadhi ya wachimbaji mchanga katika mto Mpiji wakati wa ukaguzi wa mto huo.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC lilipiga maarufu zoezi la Uchimbaji mchanga katika bonde la mto Mpiji unaotenganisha Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani ambalo limekuwa likiharibu Mazingira na kuhatarisha makazi ya watu wa eneo hilo kutokana na mmomonyoko wa udongo.

Akizungumza wakati wa ziara ya ukaguzi wa mto huo, Meneja Uzingatiaji wa Sheria NEMC Bw. Hamadi Taimuru alisema ni marufuku kwa wale wote wanaojihusisha na Uchimbaji wa mchanga katika mto huo kwa kigezo cha kusafisha mto kuendele na kazi hiyo. Aliwataka kuacha mara moja uchimbaji na kuwataka wafike katika Ofisi za NEMC ili wapatiwe vibali vyenye vigezo vya kusafisha mto na si uchimbaji wa mchanga kwa mustakabali wa utunzaji wa Mazingira.

Alisema kwa mujibu wa Sheria, ni maarufu kuchimba mchanga mita sitini ndani ya mto kwani husababisha athari kubwa kwa Mazingira na makazi zikiwemo kuhama kwa mto, mmomonyoko wa udongo na kusababisha mafuriko.



*Meneja Uzingatiaji wa Sheria (NEMC) Bw. Hamadi Taimuru na Afisa Mazingira Mwandamizi Bi. Kuruthumu Shuhu katika ziara ya ukaguzi wa Mto Mpiji ulioharibiwa na shughuli za uchimbaji mchanga.*

Kwa upande wake mwenyekiti wa Baraza la wazee Bw. Lazaro Silla alisema kwa niaba ya wakazi wa eneo hilo hawahitaji Uchimbaji wa mchanga katika eneo hilo kwani unasababisha uharibifu wa Mazingira na kuhatarisha usalama wa makazi yao hivyo ameiomba NEMC kudhibiti swala hilo ili lisiendelee kuleta madhara.

Aidha, Bw. Taimuru aliongeza kuwa marufuku hii si tu kwa mto Mpiji bali ni mito yote na maeneo yote nchini ambayo wanajihusisha na uchimbaji mchanga na kusababisha uharibifu wa Mazingira na kuhatarisha makazi ya watu.

Sambamba na hayo alisisitiza wote wanaojihusisha na Uchimbaji mchanga holela kote nchini kutii agizo hilo ili kuepusha uharibifu wa Mazingira na hatari ya kuharibika kwa makazi ili kujiepusha na adhabu kali inayoweza kutolewa.

# PROFESA MSOFE ARIDHISHWA NA UTENDAJI KAZI NEMC



Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi akimkabidhi zawadi Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Profesa Peter Msoffe mara baada ya Kikao na watumishi wa NEMC.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Profesa Peter Msoffe alionekana kuridhishwa na utendaji kazi na uwajibikaji wa watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) katika utekelezaji wa majukumu ya Mazingira hasa usimamizi wa utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Nchini.

Hayo yalidhihirika wakati alipotembelea Ofisi za Baraza jijini Dar es Salaam kwa mara ya kwanza toka kuteuliwa kwake katika nafasi hiyo ya Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Mazingira.

Alisema "NEMC pamoja na changomoto zote, bado mmepiga hatua katika suala Zima la usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira nchini.

Alisema "NEMC mnafanya kazi, watu wanaona na mnaonekana, licha ya changamoto mnazokumbana nazo, lakini endeleeni kufanya kazi kwa ajili ya manufaa ya Taifa la Tanzania, huku mkilinda Afya zenu dhidi ya Mazingira hatarishi katika Utekelezaji wa majukumu yenu" alisema Prof.Msofe.

Aidha aliainisha mambo matano ambayo watumishi wa NEMC wanatakiwa kuyazingatia katika utekelezaji wa majukumu ambayo ni kuweka uwiano kati ya vihatarishi binafsi na vihatarishi vya Mazingira ya kazi ili kuepuka madhara ya kiafya katika Utekelezaji wa majukumu, kujifunza na kushirikishana ujuzi wa utendaji kazi, ushirikiano mkubwa katika kazi na uvumbuzi katika masuala ya Mazingira ili kuweza kufanya kazi kwa kuendana na ulimwengu wa sasa.

Kwa upande wa Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi alipozungumza aliesema bado NEMC inakabiliana na changamoto katika kutekeleza majukumu yake kutokana na kukosekana kwa Sheria inayotoa Mamlaka kamili ya Utekelezaji ambapo bado mchakato wa kuifanya NEMC kuwa Mamlaka unaendelea.

Alisema Baraza linatumia vyombo vya ulinzi na usalama katika utekelezaji wa baadhi ya majukumu kutokana na kukosekana kwa Mamlaka kamili.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Profesa Peter Msoffe (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa NEMC mara baada ya kikao. Kulia kwake ni Mkurugenzi wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi na kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Utawala na Fedha (NEMC) Bw. Dickson Mjinja.

# NEMC YAINGIA MTAANI KIDIGITALI



*Kaimu Mkurugenzi Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria (NEMC), Bw. Jamal Baruti akizungumza na vyombo vya habari wakati akitoa taarifa kuhusu zoezi la Kaguzi za Mazingira linalofanyika kwa kutumia mmfumo mpya wa kidigitali wa "**Mazingira App**" katika ukusanyaji taarifa.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Halmashauri za Mkoa wa Dar es salaam limeendesha zoezi maalumu la Ukaguzi wa Mazingira kwa Miradi yote ya maendeleo kwa kutumia mfumo maalumu wa kidigitali uitwao 'Mazingira App'.

Akitoa taarifa hiyo kwa vyombo vya habari, Kaimu Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria NEMC Bw. Jamal Baruti alisema zoezi hilo litadumu kwa wiki nne na litahusisha kaguzi za Mazingira kwenye miradi ya maendeleo hususani kuangalia uzingatiaji wa matakwa ya Usimamizi wa Mazingira kama vile usimamizi wa taka, matumizi sahihi ya ardhi pamoja na uhifadhi wa vyanzo vya maji.

Aliongeza kwa kutumia mfumo wa Mazingira App pia utawawezesha kuchunguza uzingatiaji wa Sheria zinazohusu afya ya jamii, usalama wa kazi na mipango miji ambazo kwa kutokutekelezwa kwake huchangia kwa kiasi kikubwa uchafuzi au uharibifu wa mazingira.

Aidha Bw. Jamal Baruti alisema ushirikiano na uongozi wa Jiji la Dar es salaam umelenga kuongeza uelewa na ufanisi kwa maafisa mazingira kuhusu Usimamizi hafifu wa taka ngumu, changamoto ya taka za plastiki, uharibifu wa Mazingira kutokana na uchimbaji holela wa kwenye mito na mabonde na matumizi holela ya ardhi kinyume na taratibu za mipangomiji.

Kwa upande wake Meneja Kanda ya Kaskazini Mashariki (NEMC) Bi. Glory Kombe alipozungumza aliwataka Viongozi wa Halmashauri na Serikali za mitaa kutoa ushirikiano wakati wote wa zoezi hili ili kufikia tija tarajiwa kwa maendeleo endelevu ya Mazingira nchini.

Kadhalika Meneja Glory Kombe alifafanua kuwa jukumu la Halmashauri na Mamlaka za Serikali za mitaa ni kuhakikisha Miradi ya maendeleo inazingatia taratibu za Mazingira ikiwemo ufanyikaji wa Tathmini ya Mazingira na Jamii kama ilivyobainishwa kwenye Sheria ya Mazingira na Kanuni zake na kusimamia usafi wa Mazingira kwa ujumla pamoja na kuwataka maofisa Mazingira na Kamati za Mazingira kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria.

NEMC imeanzisha mfumo huo wa **'Mazingira app'** ambao ni wa kidigitali ili kurahisisha na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na uhifadhi wa Taarifa za Miradi pamoja na usajili wa Miradi mipya ambapo zitachangia Baraza na Serikali kupanga na kusimamia Miradi ya maendeleo kwa ufanisi zaidi.



*Kaimu Mkurugenzi Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria (NEMC), Bw. Jamal Baruti akizungumza na vyombo vya habari pamoja na Menejimenti ya NEMC wakati akitoa taarifa kuhusu zoezi la Kaguzi za Mazingira linalofanyika kwa kutumia mfumo mpya wa kidigitali wa "**Mazingira App**" katika ukusanyaji taarifa.*

# NEMC, KINONDONI WAADHIMISHA SIKU YA MIKOKO DUNIANI KWA KUPANDA MICHE 1000



*Meneja wa Tafiti za Mazingira NEMC Dkt.Rose Sallema akipanda mti katika zoezi la upandaji wa miti ya mikoko eneo la Kilongawima ikiwa ni sehemu ya Madhimisho ya Siku ya Mikoko duniani.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Taasisi za umma na binafsi waliadhimisha siku ya mikoko duniani kwa kupanda miche takribani 1,000 ya miti ya Mikoko eneo la Kilongawima lililopo pembezoni mwa fukwe ya 'Mbezi beach' Manispaa ya Kinondoni.

Akizungumza mara baada ya zoezi la upandaji wa miche hiyo Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Saad Mtambule aliwataka wananchi kulinda na kithamini mikoko kwani Inamanufaa mkubwa katika kulinda ikolojoa ya bahari na viumbe hai waishio majini.

Naye Dkt.Rose Sallema, Meneja wa Tafiti za Mazingira (NEMC) alipozungumza alisema mikoko ni rasilimali ya bahari inayotakiwa kutunzwa kwani inafaida kiuchumi, kijamii na kimazingira.

Naye Mkurugenzi Msaidizi, Maendeleo ya Misitu kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii ndugu. Seleboni Mushi alipozungumza aliitaka jamii kuzingatia Uhifadhi wa misitu ya Mikoko kwani husaidia kuhifadhi fukwe na hewa ukaa hivyo kusaidia kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Aliongeza kuwa ni Hifadhi ya viumbe hai na husaidia jamii hasa za Pwani katika kujipatia kipato.

Taasisi zilizoshiriki Maadhimisho hayo ni pamoja na TFS, WWF, IUCN, Wetland, Mwambao International wawakilishi kutoka maeneo ya Pwani ya Kibiti, Kilwa na Mafia.



*Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Saad Mtambule akizungumza mara baada ya zoezi la upandaji miti ya mikoko ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya mikoko Duniani.*



*Timu iliyojumuisha Taasisi mbalimbali na wananchi wakiwa katika zoezi la upandaji wa miti ya mikoko eneo la Kilongawima ikiwa ni sehemu ya Madhimisha Siku ya Mikoko duniani.*

# NEMC NA MAZINGIRA PLUS WAFANIKISHA PROGRAMU YA TAKA SIFURI KWA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA YA DAR ES SALAAM







*Baadhi ya wanafunzi wa shule maalum ya wasichana Dar es Salaam waliopata mafunzo ya Mradi wa Taka Sifuri katika picha ya pamoja na baadhi ya viongozi wa NEMC, Mazingira Plus na Halmashauri ya Wilaya ya Ubungo.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Taasisi ya Mazingira Plus walikabidhi Mradi wa Taka Sifuri kwa Shule ya Sekondari maalumu ya wasichana ya Dar es Salaam ambapo takribani wanafunzi 200 walihitimu na kukabidhiwa vyeti vya mafunzo ya mradi huo.

Hafla hiyo ya kukabidhi Mradi huo iliambatana na maonesho mbalimbali ya matokeo ya mafunzo hayo ikiwa ni pamoja na bustani za kioganiki zilizotengenezwa na wanafunzi, utengenezaji wa mbolea kupitia mabaki ya chakula, mabanda ya kuhifadhi na kutenganisha taka pamoja na sanaa ya vinyago vilivyoonesha namna viumbe hai wanavyoathirika na uharibifu wa Mazingira.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi Mradi huo, Meneja Utekelezaji wa Sheria (NEMC) Bi. Amina Kibola aliwapongeza wanafunzi hao kwa kuhitimu mafunzo hayo adhimu huku akiwasisitiza kuzingatia mafunzo hayo kwani yamebeba fursa za kiuchumi sambamba na Utunzaji wa Mazingira.

Aidha, Bi. Amina aliwasisitiza kuzingatia dhana ya punguza, tumia tena na rejeleza ambayo ni msingi wa kudhibiti uchafuzi wa Mazingira na pia ni dhana ya kuibua fursa za kiuchumi kupitia urejelezaji wa taka na uchakataji wa taka kuwa malighafi kama vile mbolea.

Kwa upande wake Mratibu wa Programu ya Taka Sifuri mashuleni Bw. Suleman Mang'uro aliwataka walimu wa Shule hiyo kusimamia na kuhakikisha mradi huo unaendelea kwa manufaa ya kiuchumi na utunzaji wa Mazingira.

# NEMC YAJA NA USAFI KAMPENI 2025




*Kaimu Mkurugenzi Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria (NEMC), Bw. Jamal Baruti akizungumza na vyombo vya habari wakati wa uzinduzi wa **"NEMC Usafi Kampeni"**.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limezindua kampeni mpya ya usafi iitwayo **"NEMC Usafi Kampeni 2025"** yenye lengo la kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika usafi wa mazingira na kuhakikisha nchi inakuwa safi, salama na yenye afya kwa wote.

Kampeni hiyo ambayo ilitekelezwa kwa ushirikiano na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, mamlaka za mikoa na Halmashauri, Taasisi binafsi, Asasi zisizo za kiserikali na wananchi, ililenga kuibua mabadiliko ya tabia na kukuza uwajibikaji wa pamoja katika kudhibiti ongezeko la uchafuzi wa mazingira, hasa taka ngumu na plastiki.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezajinwa Sheria NEMC Bw. Jamal Baruti, kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu alisema kwa sasa Tanzania inazalisha takriban tani milioni 14.4 hadi 20.7 za taka kwa mwaka, huku wastani wa uzalishaji taka kwa mtu mmoja ukiwa kati ya kilo 0.66 hadi 0.95 kwa siku. Hali hii inahitaji jitihada za dhati kutoka kwa kila mtanzania.

"Kampeni hii inalenga kuondoa dhana kuwa usafi ni jukumu la serikali pekee. Kila mtu anapaswa kushiriki, kwa kuwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 inamtaka kila mtu kuwa mdau na mlinzi wa mazingira," alisema Baruti.

Aliongeza kuwa kampeni hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050, ambayo imeweka hifadhi ya mazingira kuwa moja ya mihimili ya maendeleo endelevu. Kupitia kampeni hii, taka zitatazamwa kama fursa ya ajira kupitia miradi ya kijani, vijana na wanawake watawezeshwa kupitia mafunzo ya ujasiriamali wa mazingira, huku upandaji miti ukihamasishwa kwa nguvu zote.

Miongoni mwa shughuli zilizofanyika chini ya kampeni hiyo ni pamoja na operesheni za usafi, mafunzo ya elimu ya mazingira, mashindano ya usafi kwa shule na kata, uanzishaji wa bustani za kijani, maonesho ya bidhaa rafiki kwa mazingira, pamoja na uanzishwaji wa klabu za mazingira katika shule zote za msingi na sekondari ifikapo Juni 2026.

Lengo kuu lilikuwa ni kufikia asilimia 80 ya kaya kushiriki katika shughuli za usafi ifikapo Desemba 2025, kupunguza utupaji taka ovyo, na kuhamasisha jamii kuona taka kama rasilimali badala ya mzigo.

NEMC pia imetoa wito kwa mashirika ya maendeleo, taasisi binafsi, na wadau wengine kuunga mkono kampeni hiyo kupitia misaada ya vifaa vya usafi, miche ya miti, zawadi kwa washindi wa mashindano, pamoja na kusaidia mafunzo ya ujasiriamali wa kijani.

"Kampeni hii si ya muda mfupi. Ni wito wa Taifa kuchukua hatua za pamoja kwa ajili ya afya ya mazingira yetu na ustawi wa vizazi vijavyo. Tunachotaka ni mabadiliko ya kweli na ya kudumu," alisisitiza Baruti.

Kwa kauli mbiu isemayo "Mazingira yetu, Uhai wetu, Tuyatunze Yatutunze", NEMC inatuma ujumbe mzito wa umuhimu wa kuchukua hatua sasa, ili kulinda maisha ya sasa na baadae.



*Meneja wa Uzingatiaji wa Sheria (NEMC) Bw. Hamad Taimuru (kushoto) akielezea jambo wakati wa uzinduzi wa **"NEMC Usafi Kampeni"**..*

# NEMC YAWAFIKIA WADAU TAKRIBANI 1,450 ELIMU YA MAZINGIRA MAONESHO YA NANENANE

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limewafikia wadau takriban 1,450 kwa utoaji wa elimu ya uhifadhi na usimamizi endelevu wa mazingira katika Maonesho ya Kilimo ya Nane Nane jijini Dodoma na Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya mwaka huu.

Elimu hiyo imetolewa kwa wadau kutoka sekta mbalimbali ikiwa ni sehemu ya juhudi za Baraza hilo kuhamasisha uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa kulinda mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Katika banda lake la maonesho, NEMC ilielimisha kuhusu mbinu bora za kilimo hifadhi kinachozingatia mazingira, ufugaji endelevu, uvuvi salama pamoja na kulinda vyanzo vya maji.

Aidha, wananchi na wadau waliotembelea hapo walielimishwa kuhusu umuhimu wa kufanya tathmini ya athari kwa mazingira kabla ya kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo hususani ya kilimo ili kupunguza athari hasi kwa mazingira.

Miongoni mwa masuala yaliyopatiwa kipaumbele ni pamoja na kuwahimiza wawekezaji kusajili miradi NEMC ili kupata vyeti vya mazingira kama kigezo muhimu cha kuendesha shughuli zao kisheria na kwa kuzingatia mazingira.

Katika maonesho hayo, wataalamu wa NEMC pia walieleza athari za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja za shughuli za binadamu kama uchomaji moto hovyo, ukataji miti na utupaji taka kwenye mifumo ya ikolojia, hali inayochangia mabadiliko ya tabianchi, mmomonyoko wa ardhi na upungufu wa rasilimali maji.



*Elimu ya Mazingira ikitolewa kwa wageni waliotembelea banda la NEMC katika Maonesho ya Wakulima, Nanenane 2025 yaliyofanyika katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.*




*Afisa Mazingira (NEMC) Bw. Bakari Issa Mwaruma akitoa elimu ya Mazingira kwa wageni waliotembelea banda la NEMC katika Maonesho ya Wakulima, Nanenane 2025 yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya.*

"Tunawahimiza wawekezaji kushiriki kikamilifu katika kulinda mazingira. Elimu tunayoitoa ni msingi wa kufanya maamuzi sahihi ya kisera, kiuchumi na kijamii yanayozingatia mustakabali wa mazingira yetu," alisema Bi. Dalia Kilamlya, Afisa Mazingira (NEMC).

Kwa ujumla, mwitikio wa wadau mbalimbali katika kupata elimu ya mazingira kutoka NEMC ulionekana kuwa mkubwa na wenye kuleta matumaini ya mabadiliko chanya katika namna jamii inavyoshiriki kwenye kulinda na kuhifadhi mazingira.

# NEMC YASHIRIKI HAFLA YA UFUNGAJI WA MAONESHO YA NANENANE, DODOMA




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza wakati wa hafla ya ufungaji wa Maonesho ya Wakulima (Nanenane 2025) katika viwanja vya Nzuguni, jijini Dodoma.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilishiriki kikamilifu kwenye hafla ya ufungaji wa maonesho ya 32 ya wakulima (Nanenane) Kitaifa yaliyofanyika katika viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt Samia Suluhu Hassan ambapo katika hotuba yake alisisitiza umuhimu wa kilimo bora na endelevu kama mhimili wa maendeleo ya Taifa.

Alisema sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi ndio uti wa mgongo wa uchumi wa nchi, hivyo zinahitaji uwekezaji wa kutosha, ubunifu na usimamizi madhubuti ili kuijenga kesho bora kwa Watanzania wote.

Alielekeza Wizara ya Kilimo kuimarisha upatikanaji wa pembejeo bora kwa wakulima, pamoja na kuunganisha nguvu katika kukuza sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Mhe.Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan alitangaza kuongeza siku mbili zaidi za maonesho hadi tarehe 10 Agosti ili kutoa nafasi kwa wananchi na wadau kuendelea kupata huduma na elimu mbalimbali.

" Maonesho haya ni siku nane, lakini kiuhalisia siku nane hazitimii kwani maandalizi yanachelewa, hivyo kuanzia mwaka ujao maandalizi ya maonesho yaanze tarehe 25/07." Ameelekeza Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan

Hafla hiyo ya ufungaji ilihudhuriwa pia na viongozi mbalimbali wa Serikali wakiwemo Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu, Wakuu wa Mikoa ya Dodoma na Singida, Wakuu wa Taasisi za Serikali na Binafsi.


Kwa upande wake, NEMC ilitumia maonesho haya kutoa elimu juu ya uhifadhi wa mazingira katika shughuli za kilimo na ufugaji, ikiwa ni pamoja na matumizi salama ya mbolea, upandaji miti, na ulinzi wa vyanzo vya maji.

Maonesho ya Nanenane mwaka huu yaliendelea kuwa jukwaa muhimu kwa serikali, Taasisi na wananchi kushirikiana katika kuendeleza kilimo chenye tija na rafiki kwa mazingira.



*Baadhi ya watumishi wa NEMC wakiwa katika hafla ya ufungaji wa maonesho ya wakulima (Nanenane 2025) katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma*

# Kauli ya Mazingira Yetu
















*Wasiliana nasi;*

**Mkurugenzi Mkuu,**

**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),**

Ghorofa ya 6, Jengo la Kambarage, Barabara ya PSPF S.L.P 2724, Dodoma, Tanzania.

**Simu:** +255 26 296 0098, +255 713 608 930,

Barua pepe: dg@nemc.or.tz, Tovuti: www. nemc.or.tz

Namba ya Bure: **0800 110 115**

Whatsapp: +255 680 400 400

@nemctanzania

NemcTVTanzania

www.nemc.or.tz

**#MazingiraYetuUhaiWetu**